

# »Sifa za dume bora«

Dume ni muhimu katika kuzaliana. Kwa hivyo apaswa kuchaguliwa kwa uangalifu.

Dume huthaminiwa zaidi kuliko jike kwa sababu anaweza kuhamisha sifa zake bora kwa mifugo mingine. Kwa mfano, dume mmoja anaweza kuhudumia hadi majike 50 katika kipindi cha miezi 3 ya kuzaliana. Unapochagua dume kwa ajili ya kuzaliana, lazima awe na sifa bora, laa sivyo anaweza kueneza sifa duni katika kundi lako.

## Aina safi/ chotara.

Dume kuwa na rangi nyeupe haimaanishi kwamba ni chotara au safi. Wanyama wa kienyeji wana uwezo wa kuwa na rangi yoyote.

Aina chotara hupendwa sana kwa sababu hukua haraka. Kupandishana aina safi na ya kienyeji huhamisha sifa bora ya utumiaji mzuri wa malisho kwa watoto. Aina za kienyeji huchukua muda mrefu zaidi kufikia 70kg na hicho ndicho kiwango cha juu wanachowezu kufikia, huku aina safi huchukua muda mfupi kufikia 70kg na wanawenza kufikia hadi kilo 120.

Aina safi zina pua za kirumi (pua zenye ncha kali) na pembe zao huunda nusu duara na uso. Masikio yao ni makubwa na mrefu zaidi kupita midomo.

## Madume kwa ajili ya kuzaliana

Dume kuwa mkubwa haimfanyi kuwa anafaa kutumika kwa kuzaliana. Mapumbu ya dume mzuri lazima yawe na ulinganifu na yasiwe mrefu sana.

Madume wakuzaliana wanapaswa kuwa na mikia iliyosimama na wawe na rangi maalum. Hii husaidia kutambua aina yake.